**Masomo ya Biblia**
**kwa**
**KANISA LA ELOHIM (COG)**
**Siku Ya Saba (7th day)**

---

**Robo Ya Pili**

**2016**

---

**Ya**

**Aprili, Mei, Juni.**

**Kutumiwa na Biblia**

---

**Mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache...**

---

**Tuma maombi yote kwa S.L.P 568,**

**Jerusalem - Israel**

**-------------------------------------------------------------**

**Somo La Aprili 2, 2016.**

## KUZALIWA UPYA

**Somo Kuu: Yohana 3.**

**Fungu La Kukariri: Yohana 3:8.**

1. Kuna wale waliovutiwa na Mwokozi kupitia miujiza yake wakati wa Pasaka. Ni neno lipi mmoja alisema kwa Mwokozi? Yohana 3:1, 2.

2. Ni nini Masihi alielekeza mawazo yake? Yohana 3:3.

3. Ni nini kinachoonyesha kwamba Nikodemo alishangazwa na jambo hili? Yohana 3:4.

4. Mwokozi alisisitiza vipi umuhimu wa ujumbe wake? Yohana 3:5.
5. Ni mfano gani Yeye alitumia kusisitiza somo hili? Yohana 3:6-8.

**MAONI**: Neno "tunajua" linaonyesha kwamba Nikodemo hakuwa akimtafuta Bwana yeye peke yake. Mwokozi alikuwa amebaini utukufu wake katika Kana ya Galilaya na huko wakati wa Pasaka uwezo wake kama mwakilishi wa Elohim ilidhihirishwa wazi. Wafarisayo hawakuwa wanyenyekevu wa kutosha kumtafuta mchana, huyu mkuu alikuja usiku. Yeye akashangazwa kama wengi walivyo leo kuhusu ni nini maana ya kuzaliwa upya; bado Mwokozi anasema kwamba uzoefu huu ni muhimu kama njia pekee ya kupata Ufalme.
6. Ni jambo lipi lingine Nicodemo aliuliza? John 3:9.
7. Mwokozi alimjibu vipi juu ya swala hilo? Yohana 3:10-13.
8. Ni awamu gani nyingine ya mafundisho Mwokozi alianzisha? Yohana 3:14, 15.
9. Kwa nini Elohim alimpa mwanawe kwa ulimwengu? Yohana 3:16.
10. Ikiwa imani katika Mwokozi huleta wokovu, ni nini kwamba huleta hukumu? Yohana 3:17-19.

******************************

**Somo La Aprili 9, 2016.**

## IMANI - HITAJI LA WACHAJI ELOHIM

**Somo Kuu: II Wakorintho 4: 1-18.**
**Fungu La Kukariri: Waebrania 4: 2.**
1. Ili kumpendeza Elohim, ina tulazimu tumiliki nini? Waebrania. 11: 6.
2. Ni wapi kwa mara ya kwanza iliandikwa tendo la imani katika upatanisho wa damu ilifanyika? Ebr. 11:4.
3. Ni tendo gani la imani lilihitajika jioni ya Pasaka? Kutoka. 12:7.
**MAONI**: Kuchinjwa kwa kondoo ya Pasaka ilikuwa haitoshi, ilikuwa hadi kila mmoja kujua kama damu ilikuwa imepakwa kwa miimo miwili ya mlango wa nyumba. Haitoshi leo kujua kwamba Masihi aliishi na kufa, kwa kila mtu binafsi lazima apokee mwenyewe sadaka Yeye alitolewa kwa ajili yao.

4. Katika siku zilizopita, kwa nini neno halikuwa na faida kwa Wana wa Israeli? Waebrania. 4:2.
5. Jinsi gani Mwisraeli alionyesha imani katika upatanisho wa damu? Mambo ya Walawi. 4: 27-30.
6. Ni ufafanuzi gani Biblia imetoa kwa  jina imani? Warumi. 12:3.
7. Ni wangapi waimiliki imani hii? Warumi. 12:3.
8. Kwa nini watu wengi upiga kelele, ambayo inaonyesha ndani yao ukosefu wa imani? Yohana 6:30.
9. Kabla hatujauona utukufu wa Elohim, ni lazima tufanye nini? Yohana 11:40.

**MAONI**: Yahshua angeweza kusema neno na jiwe lingeondoka chini ya udhibiti wa Elohim, lakini alichagua kutumia nguvu za kibinadamu kama inavyowezekana. Kwa ombi lake katika Yohana 11:39, ilionekana ukosefu wa imani katika moyo wa Martha. Baada ya nguvu za kibinadamu kufika kikomo chake, katika Yohana 11:41, Alitoa wito kwa Baba wa kufanya kile uwezo wa binadamu haukuweza kufanya; kufufua maiti. Tukiongea kwa kiroho, Elohim peke yake anaweza kutufufua kutoka wafu na uozo wa kiroho.

10. Kwa nini Yahshua alimpongeza huyo ofisa kupita wengine? Mathayo. 8:5-8.
11. Ni nini hutuongoza kuamini kwamba Masihi atarudi hivi karibuni? Luka 18:8.
12. Ni nani tu atapokea hitaji kamili la Elohim? Ufunuo 14:12.

*******************************

## Somo La Aprili 16, 2016.

## TUMETEULIWA KUMSIFU

**Somo Kuu: Zaburi 117.**

**Fungu La Kukariri: Zaburi 117: 1.**

1. Je, kusifu ni sehemu ya Utumishi? I Mambo ya Nyakati 16:4; 23: 5.
2. Ni mfano gani uliotolewa kwetu sisi katika I Mambo ya Nyakati 23:30 kuhusu kusifu?
3. Je, muziki ni njia inayofaa ya kumtukuza? II Mambo ya Nyakati 7: 6.
4. Je inafaa tumsifu kwa sauti zetu? II Mambo ya Nyakati 20:19.
5. Je inafaa tumsifu kwa kuimba? I Mambo ya Nyakati 13: 8 soma pia II Mambo ya Nyakati

20:21.

6. Ni nguvu ipi, tumeonyeshwa kupitia sifa katika II Mambo ya Nyakati 20:22?

7. Tunapaswa kumsifu vipi na tunapaswa kuonyesha nini? Zaburi 9:1.

8. Je, tunafaa kumsifu kwa shukrani? Zaburi 28:7.

9. Ni vazi gani tunapaswa kuvaa katika uhusiano na sifa? Isaya 61:3.

10. Ni nani ameamuriwa kumsifu Bwana? Warumi 15:11.

**MAONI**: Sifa ni imenakiliwa kote katika maandiko kama sehemu muhimu ya kumtumikia Mwenyezi. Mfalme Daudi alipata nguvu kubwa katika kumsifu Bwana. Sifa za Israeli zilifika katika kiti cha enzi cha Baba muda kwa muda na miujiza mingi ilifanyika kama matokeo. Na Roho wa Baba atufundishe jinsi ya kumtukuza ili dunia nzima imsikie na imjue.

******************************

**Somo La Aprili 23, 2016.**

## OMBENI BILA KUKOMA

**Somo Kuu: Zaburi 66: 13-20.**

**Fungu La Kukariri: Zaburi 6: 9.**

1. Je, Bwana ayasikia maombi ya watu wake? Mithali 15:29.

2. Je atayasikia maombi yetu  ikiwa tutaendelea kutotii tukijua? Mithali 28:9.

3. Tunaweza kupata nini kupitia njia ya maombi? Mathayo 21:22.

4. Je Masihi amesema nini kuhusu maombi ya unafiki? Mathayo 23:14.

5. Ni mifano gani mizuri tumepewa ili tuifuate katika Matendo 1:14 na 6:4?

6. Ni mara ngapi tunafaa kwenda mbele za Bwana katika sala? Waefeso 6:18; pia soma Waroma 12:12 na Wakolosai 4:2.

7. Je, tutafanya nini kama ndugu au dada anapitia kwa njia ya majaribio? Matendo 12:5.

8. Ina umuhimu gani maombi yaliyo ya imani? Yakobo 5:15.

9. Tutawezaje kila siku kujenga, kuinua, na usaidizi kwa mahitaji ya kila mmoja wetu? Yakobo 5:16.

**MAONI**: Biblia inatuambia "tukeshe na tuombe". Mafanikio makuu yanaweza kupatikana kwa

maombi ya watu wake. Tuendelee kusali, kama amri ya Biblia inavionyesha, kwa amani ya Yerusalemu, kwa viongozi wa mataifa yetu na kwa ajili ya ndugu na dada duniani kote.

******************************

**Somo La Aprili 30, 2016.**

**MFANO WA MMASIHI**

**Somo Kuu: Wafilipi 4: 1-13.**

**Fungu La Kukariri: Wakolosai 3:12.**

1. Ni nani ni tunawakilisha na ni kwa namna gani? 1 Timotheo 4:12.
2. Ni nani ni tumeagizwa kufuata kama mfano wetu? Marko 8:34.
3. Ni kina nani tumetolewa kama mifano ya uvumilivu? Yakobo 5:10, pia ona 1 Petro 2:21.
4. Ni mtazamo gani dunia inafaa kuona katika sisi baada ya kuwekwa katika majaribu? 1 Petro 4:16.
5. Ni nini nia zetu zafaa kutafakari ili kutufanya mifano bora? Wafilipi 4:8.
6. Ni kwa njia gani tunapaswa kuwasiliana mmoja kwa mwingine? Waefeso 4:29.
7. Tufaa kujivika nini? Wakolosai 3:12.
8. Je, ni baadhi ya mambo yepi tunaambiwa tuyafuate ili tuwe mifano mizuri zaidi katika maisha yetu? Warumi 14:19, pia ona 1 Timotheo 6:11.

**MAONI**: Nyakati nyingi sisi husahau kwamba twafaa kuwa mwanga wa dunia, na twafaa kufuata mifano tuliyoachiwa katika Neno la Elohim. Kwa mfano wetu wa maisha ya umasihi tutaweza kuvuta nafsi nyingi kwa Ufalme. Kwa hivyo ni muhimu sana kuwa mfano bora tunapoweza na kuomba kila siku kupata roho kama ya Masihi.

******************************

**Somo La Mei 7, 2016.**

**KUSINGIZIA NA KUONGEA UOVU**

Hakuna mtu anapenda kusengenywa, wala hakuna mtu yeyote hufurahia kusingiziwa. Hata hivyo ni hakika hakuna uhaba wa wambeya au wasingiziaji. Hii inaonyesha kwamba wengi hawana chuki halisi kwa ajili ya michezo yenyewe, na kwamba ni wakati tu wao wenyewe huwa malengo ya mishale yake ya uchungu wao ufahamu kikamilifu unyarafu wake. Wakati mwingine tunajikuta tukishiriki katika aina yoyote ya "kuzungumza mabaya" au uvumi usio na huruma, tunafaa kufanya vizuri kuchunguza nia zetu. Tungefaa pia kufanya vizuri tujiulize kama sisi kweli tunajua nini tunazungumzia. Mara nyingi watu hurudia mambo ambayo hawana ukweli dhabiti. Wanaweza hata kutojua mtu ambaye wanasingizia, lakini wamesikia tu "hili na lile" kutoka kwa baadhi ya "mwandani wake." Mwandani huyu mara nyingi, katika hali halisi, ni "mgeni" – ni kwa sababu hii yeye uanza kusingizia! Kwa hakika, baadhi ya nia kuu za kusingizia ni hisia za kujiona duni na wivu, ambao uletwa juu ya hali dhaifu ya kiroho na haja ya kuhalalisha mtu binafsi kwa kusingizia wengine.

**Somo Kuu: Waefeso sura ya 4.**

**Fungu La Kukariri: Waefeso 4:29.**

1. Ni nini chanzo cha kusingizia? Mathayo 15:19; Luka 6:45.
2. Je, tunafaa kuwaamini wale ambao ujiingiza katika kusingizia? Yeremia 9:8.
3. Nini kundi lipi la watu hufurahia kusengenya? Mithali 11: 9; Zaburi 50:20; Yeremia 6:28.
4. Ni athari gani za kusingizia? Mithali 6:19.16: 28, 18: 8, 26:20.
5. Mwisho wa umbeya unaoudhi, maongezi yenye ladha, maneno yaliyotiwa chumvi na uvumi ni nini? Mhubiri 10:12-14.
6. Je, sisi tutahalalishwa tukiongea maneno mabaya kwa watu fulani ambao tunadhani wanastahili hayo maneno? Tito 3:2-8.
7. Je, tutahitajika kutoa hesabu ya maneno yetu yote ambayo si ya kweli na yenye kudhuru? Mathayo 12:36,37.
8. Je, watu wanaonekana wachaji Elohim, wakati mwingine uanguka katika dhambi ya kusingizia na kuzungumza mabaya? Yakobo 1:26.
9. Ni kuhitimu kupi kunaohitajika kwa wale ambao Bwana ataruhusu ndani ya hema lake? Zaburi 15:1-3.

******************************

**Somo La Mei 14, 2016.**

**UOVU**

Booker T. Washington mara moja alisema, "Mimi najitahidi kutoruhusu mtu yoyote kufupisha au kuharibu roho yangu kwa kunifanya nimchukie." Chuki na nia mbaya ufanya tu hivyo - uharibu, uichafua na kuharibu roho. Kama wamasihi tunapaswa kuepuka uovu, si tu kama sumu hatari ambayo uua ukuaji wa kiroho, lakini pia kama kinyume cha Elohim.

**Somo Kuu: Wakolosai 3:1-17.**

**Fungu La Kukariri: Wakolosai 3:8.**

1. Ni hitaji gani linalohitajika kwa ukuaji wa kiroho? 1 Petro 2:1,2.
2. Ni pamoja na nini ibada haiwezi kuwa sahihi? Yakobo 3:9-18.
3. Uovu tu kidogo unaweza kunajisi mwili mzima? 1 Wakorintho 5:6-8.
4. Je, twafaa kuwaheshimu watu wote, au ni haki kuwa na nia mbaya kwa wasioamini? 1 Petro 2:12-17.
5. Ni wanaume gani wamchao Elohim huwa bila kinyongo kwa maadui zao? Ayubu 31:29,30; Zaburi 35:11-14.
6. Je, Masihi hutuambia tufanye nini kwa wale ambao hututumia kwa njia isiyo na haki? Mathayo 5: 43,44.
7. Ni mwisho gani kwa wale hufanya njama ya kuwadhuru wengine? Zaburi 7:14-16.

******************************

**Somo La Mei 21, 2016.**

**UBISHI - ZANA YA SHETANI**

"Nyumba ambayo imegawanyika makundimakundi yanayopingana haiwezi kudumu," Masihi alisema. Huu ni ukweli maalumu hasa unaotumika kwa Kanisa leo. Ugomvi na mgawanyiko umejaa kila mahali na ni zana ambazo Shetani anatumia kufanya watu wa Elohim wawe wadhaifu. Biblia inafundisha kwa ushupavu dhidi ya ugomvi na ubishi kati ya ndugu. Masihi huangalia watu ambao hufuata mfano wake katika upendo wa kindugu. Masihi alijihusisha sana kuhusu jambo hili katika maombi yake kwa wafuasi wake. Hamu yake kuu ni kwamba, "Wote wawe na umoja kama wewe, Baba, ulivyo ndani yangu, nami ndani yako; hao nao wawe ndani yetu; ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma. Nami utukufu ule ulionipa nimewapa wao; ili wawe na umoja kama sisi tulivyo umoja. . .Mimi ndani yao, nawe ndani yangu, ili wawe wamekamilika katika umoja "(Yohana 17:21-23).

Ushahidi wa umoja wetu utasababisha dunia ijue kwamba Injili ambayo tunakiri ni ya kweli. Kwa upande mwingine, ikiwa watu wa Elohim watajulikana kwa ubishi na ugomvi, hii itakuwa onyesho mbaya juu ya Masihi. Tunapojifunza kile Biblia inasema juu ya somo hili muhimu, hebu tujitahidi kusafisha mioyo yetu kutokana na mawazo yote yenye utata na kuungana katika mapenzi kamili ya Elohim.

**Somo Kuu: 1 Wathesalonike 5: 9-15.**

**Fungu La Kukariri: 1 Wakorintho 11:16.**

1. Nini husababisha mapigano na ubishi? Yakobo 4: 1; Mithali 26:21; Mithali 22:10; Mithali 13:10.

2. Je, hata baadhi wanaokiri Masihi hupanda mbegu za fitina? Wafilipi 1:15-16.

3. Je, Biblia hukubali mijadala juu ya masuala madogo ya mafundisho? Tito 3:9.

4. Je, unapaswa kufanya nini wakati mtu mwingine hutoa changamoto kwa namna yenye utata? 1 Petro 3:8-11.

5. Nini tofauti kati ya mtu mwenye hekima machoni mwa Elohim? Yakobo 3:13-18.

6. Nini tofauti kati ya mtu mpumbavu? Mithali 18:6-8.

7. Ni nini kinachofananishwa na amani? Marko 9:50.

**MAONI**: Katika maandiko hapo juu, amani hulinganishwa na ladha ya chumvi. Kama vile chumvi bila ladha yake ni bure, hivyo Injili bila amani ni bure na haiweze kufanya kazi, na huwa kama kumeza kidonge kichungu.

8. Dunia itajuaje kwamba sisi ni watoto wa Elohim? Mathayo 5:9.

******************************

**Somo La Mei 28, 2016.**

## HATARI YA TAMAA

**Somo Kuu: Luka 12: 13-32.**

**Fungu La Kukariri: Luka 12:15.**

**MAONI**: Ufafanuzi wa " Tamaa" ni: " kutamani kuliokithiri, au kupita kiasi hamu ya kupata na kumiliki " --Webster.

1. Nini ilionyesha kanuni hii kuwa na nguvu katika mtu huyu tajiri ambaye tayari alikuwa na zaidi ya kutoweza kutunza? Luka 12:18,19.
2. Je Bwana huita wanaume kama hawa vipi, na alisema nini kwake? Luka 12:20.
3. Nini hitimisho ambayo Mwokozi hutoa kutokana kwa mfano huu? Luka 12:21.
4. Je, mtume Paulo huita tamaa aje? Wakolosai 3:5.

**MAONI**: Moja ya amri kumi inakataza tamaa, na tumeamriwa hapa "vifisheni" au kuharibu dhambi ya kutamani, ambayo huhesabiwa pamoja na dhambi ambazo watu kwa ujumla huchukia.

5. Je, tunaambiwa huja nini juu ya watu wanaotenda dhambi zinazohesabiwa katika fungu hili? Wakolosai 3:6.
6. Tamaa ilisababishaYuda kufanya nini? Marko 14:10.11.
7. Ni tofauti gani kati ya njia ya watu waovu na Bwana huona mwenye tamaa? Zaburi 10:3.
8. Nini moja ya mahitaji maalum Musa alidai katika wale watu tajiri alitakiwa kuchagua kwa watawala katika Israeli? Kutoka 18:21; 1 Timotheo 3:2-3.
9. Ni nini ilisemwa kuhusu tamaa, kama moja ya ishara za siku za mwisho? II Timotheo 3:1-2.
10. Wakati dhahabu, fedha, mali, dhamana na utajiri mkuu hukusanywa na kuwekwa, itamfanya nini mtu katika siku hizi za mwisho? Yakobo 5:3.
11. Je, ni nini watumishi na viongozi waliamuriwa kufanya ili kujiweka wazi wenyewe, na kutekeleza wajibu wao kupitia hali kama hiyo? 1 Timotheo 6:17-19.

12. Ni kwa njia gani Mwokozi alisema kuhusu tamaa? Luka 12:15.

******************************

**Somo La 4 Juni 2016.**

**DHAMBI NA SULUHISHO?**

**Somo Kuu: Kutoka 20:1-21.**

**Fungu La Kukariri: Yakobo 2:10.11.**

1. Je, dhambi inajulikana kama nini? 1 Yohana 3:4.
2. Dhambi za watu ziliondolewa vipi katika nyakati za kale? Mambo ya Walawi 5:14,15; Mambo ya Walawi 7:11,37,38.
3. Ikiwa mtu alikuwa maskini mno kumudu kondoo, basi kile ambacho ni lazima wangeua badala, kwa ajili ya upatanisho wa dhambi zao ni nini? Mambo ya Walawi 6:6,7.
4. Ni wakati gani kulikuwa na kipindi maalum kimewekwa kando kwa ajili ya Israeli ili kufanya upatanisho kamili kwa ajili ya dhambi waliyofanya wakati wa mwaka? Hesabu 29:12.
5. Ni wanyama wengi vipi walikuwa sadaka siku ya kwanza ili kuondoa dhambi? Hesabu 29:13.
6. Ni wangapi waliuawa kila siku katika kipindi hiki cha upatanisho? Hesabu 29: 17,20,23,26,29,32,35,36.
7. Kwa nini waliwaua wana-kondoo hawa wasio na hatia na ni kwa nani kipindi hicho cha upatanisho kililenga? Yohana 1:29-36 1 Petro 1:19.
8. Ilikuwa ni sheria ya amri kumi ambayo ilipigwa marufuku na kuachwa au ilikuwa ni mfumo huu wa kale wa msamaha ulimalizika? Waebrania 10:3-12.

**MAONI**: Tunaposoma kuhusu mateso ya Mwokozi wetu juu ya mti na kutazama uchungu wa kusulubiwa kwake, tunapaswa kuwa na hisia katika njia sawa kwamba watu waliona juu ya mauaji ya wana-kondoo wasio na hatia, kama sadaka zao kwa ajili ya dhambi zao. Jambo hili linafaa litufundishe matokeo ya kutisha ya kutomtii mkuu, na Mwenyezi, ambaye aliumba ulimwengu, na alituumba kwa mfano wake mwenyewe. Inatupasa kuelewa kwa ukamilifu kwamba kuvunja sheria hii kulileta kifo cha Mwana-kondoo mpendwa wetu na Mwokozi msalabani, sawa tu kama kusababisha kifo cha wanyama hao, hizo siku za kale. Alimwaga damu

yake na alitoa maisha yake kwa ajili yetu ili atuokoe kutokana na adhabu ya kifo, na yeye hakufa kuitangua sheria yoyote. Anasema "Sikuja kuitangua sheria au manabii, bali kutimiliza ..." (Mathayo 5:17). Unabii na sheria ambazo zilinena kuja kwake na kifo zilitimia, na kumalizika na kiwango cha juu. Zilitimiza lengo lake na kuisha lakini hazikutanguliwa.

9. Ilikuwa kwa muda mrefu kiasi gani Masihi aliyeahidiwa, na Mwokozi wa Israeli, atakuja ulimwenguni? Isaya 7:14.

10. Ilikuwa Yeye atolewe kama mwana-kondoo, kwa dhambi za watu? Isaya 3:7,8.

**MAONI**: Wayahudi leo ambao wamekuja Israeli, kwa ujumla wanailewa dhambi, na huogopa uwezekano wa kufa kabla ya wakati wa upatanisho katika mwezi wa saba. Bado wanaendelea kusherehekea jambo hili kila mwaka kwa kujifunga, lakini si kwa uuaji wa wanyama kama ilivyokuwa katika siku za zamani. Biashara zote za Wayahudi husimamishwa katika Israeli; ila tu usalama na mifumo ya dharura ufanyika.

11. Je, amri bado zafaa kutunzwa kwa mujibu wa Agano Jipya? 1 Yohana 2:1-4, na 5:3, pia Ufunuo 12:17, na 22:14.

******************************

**Somo La 11 Juni 2016.**

**ONYESHO LA WEMA WA MBINGUNI NA NGUVU ZA UPONYAJI**

**Somo Kuu: Mathayo 9:20-38.**

**Fungu La Kukariri: Mathayo 9:22.**

1. Nani alionyesha imani kubwa kwa ajili ya uponyaji? Mathayo 9:20.
2. Ni uzoefu gani yeye alikuwa nao kabla ya hili jambo? Marko 5:25,26.
3. Je, alikuwa na kiasi kikubwa cha ujasiri? Marko 5:27,28.
4. Wakati yeye aligusa Bwana Yahshua, matokeo yalikuwa nini? Marko 5:29.
5. Kwa nini Yeye alitambua mguso huu? Swali lake lilikuwa ni nini? Marko 5:30.
6. Wanafunzi waliliona swali hili namna gani? Marko 5:31.
7. Jinsi gani Mwanamke alijisikia kuhusu hilo swali? Marko 5:33.
8. Ni maneno gani ya faraja yalisemwa kwake na Masihi Yahshua? Marko 5:34; Mathayo 9:22.

**MAONI**: Hili ni jambo la kipekee, ambalo mmoja alipona bila kushughulisha Bwana. Hii ni kwa sababu ya wema ambao ulikuwa ndani yake. Tukiwa wafuasi wa Masihi sisi tutamiliki huo wema wa Mbinguni - Roho Mtakatifu - kwa kiasi kwamba hata wakati sisi hatufahamu hayo, wengi wanaotukaribia wataimarika na Roho wa Elohim anayezuru ndani yetu.

9. Ni miujiza gani iliyofuatiwa na uponyaji wa kutokwa damu? Mathayo 9:23-25.
10. Ni nini vipofu wawili walitaka kutoka kwa Bwana? Mathayo 9:27.
11. Waliendelea kutarajia kuponywa kwa muda gani? Mathayo 9:28 (sehemu ya kwanza).
12. Ni swali gani Yahshua aliwauliza? majibu yao yalikuwa yepi? Mathayo 9:28 (sehemu ya mwisho).
13. Katika kuwaponya, Yahshua aliamru nini? Mathayo 9:29-30.
14. Waliona hiyo amri vipi? Mathayo 9:31.

**MAONI**: Baraka za uponyaji zilileta furaha kwa mioyo yao ambayo hakuna kitu kingeweza kuikandamiza.

15. Ni nani aliletwa mbele yake Yahshua kwa ajili ya uponyaji? Mathayo 9:32.
16. Ni nini kilichotokea wakati pepo alipotolewa? Mathayo 9:33.
17. Uamuzi wa Mafarisayo kuhusu hili jambo ilikuwa nini? Mathayo 9:34.
18. Yahshua alishirikishwa daima vipi? Mathayo 9:35.
19. Hali ya kiroho ya watu ilimwathiri Yahshua jinsi gani? Mathayo 9:36,37.

**MAONI**: Naam, kwamba Elohim angeweza kupata wanaume/wanaweke zaidi wa kutumia leo kwa ajili ya uponyaji wa wagonjwa na wa kuhubiri Injili! Wanaume/wanawake wanayo huruma ya Masihi. Hii haitakuwa rahisi mpaka kuwe na uamsho wa upendo wa Elohim katika mioyo; mpangilio ni kwamba nguvu zitafuata ndani ya nafsi. Nguvu za huruma, nguvu kwa ajili ya huruma; uwezo wa kulia juu ya wagonjwa na ambao si waamini, kama vile Masihi Yahshua alilia kaburini la Lazaro.

******************************

**Somo La 18 Juni 2016.**

**MAISHA YA MITUME**

**Somo Kuu: Matendo 2.**

**Fungu La Kukariri: Matendo 2:42.**

1. Ni mfano gani Mtume Petro alisema kwamba wafuasi wa Bwana wanatakiwa kufuata? I Petro 2:21; I Yohana 2:6; Waefeso 5:1.

2. Katika kufuata nyayo za Yahshua, ni bidii na shauku gani waliokuwa nayo mitume wa Yahshua; katika kuitikia mwito wa mbinguni? Mathayo 4:18-22; Marko 10:28.

3. Baada ya kuacha kujishirikisha wao binafsi (kazi) kwa ajili ya Injili, jinsi gani baadhi, ambao walikuwa watumishi na viongozi wa juu wa serikali ya nchi yao waliitikia? Luka 5:27-32; Wafilipi 3:7,8; Luka 19:1-8.

4. Ni kupitia nini hawa wanafunzi waliojitolea kwa Yahshua walipata kujimudu katika maisha yao? I Wakorintho 4:12; Matendo 18:3.

5. Kulikuwa na kauli moja na umoja wa akili na moyo katikati yao? Matendo 4:32; 2:46.

6. Je, mitume walikuwa na mtazamo gani kuhusu maafa na ustawi wa wenzao na ndugu? Waefeso 1:15-19.

7. Jinsi gani wao waliteseka kwa ajili ya Yahshua na Injili? Waebrania 1:36-38.

8. Walikuwa na ukarimu kiasi gani? Matendo 2:45; 4:32.

9. Jinsi gani wao wenyewe waliishi kwa nafsi ambazo zilizovutwa kwa Bwana kwa njia ya mahubiri yao? 1 Wathesalonike 2: 2; 5: 7-10.

10. Mtazamo wao juu ya mateso, taabu na wale ambao waliwatendea vibaya ulikuwa upi? Matendo 5: 40,41; 2 Wakorintho 12:10.

11. Jinsi gani Mathiya alihesabiwa pamoja na idadi ya wale mitume kumi na mmoja? Ilikuwa ni kwa upendeleo, uteuzi, ubaguzi, upigaji kura au kwa kutolewa kura (casting of lot)? Matendo 1:23-26.

12. Jinsi gani walivyoona kukusanyika pamoja kwa ndugu? Matendo 2:42-46.

******************************

**Somo La 25 Juni 2016.**

**UJUMBE WA MWISHO WA PAULO KWA KANISA**

**Somo Kuu: 2 Timotheo 4:1-8.**

**Fungu La Kukariri: 1 Timotheo 5:7**.

1. Ni kwa nani Paulo alikabidhi maagizo yake ya mwisho, na ni kwa wakati upi yeye alisema walio hai na wafu watahukumiwa? 2 Timotheo 4:1.

2. Je, yeye aliwaagiza nini watu wake kuhubiri, na matumizi ya mafundisho ni nini? 2 Timotheo 4:2.

3. Ni unabii gani alitoa wa mitizamo ya watu juu mafundisho ya kweli? 2 Timotheo 4:3.

4. Jinsi gani yeye alisema watu wa siku za mwisho kwa ujumla watakuwa wakizingatia ukweli, na watageukia nini? 2 Timotheo 4:4.

5. Jinsi gani yeye alimfundisha Timotheo kuhusu taabu katika kazi iliyo mbele yake? 2 Timotheo 4:5.

6. Je, Paulo alikuwa ametoa uamuzi kuhusu hatma yake na kuwa tayari kuyatoa maisha yake? 2 Timotheo 4:6.

7. Je, alikuwa ameridhika kabisa na vita vya maisha yake ambayo daima alipigina, na alijua kwamba alikuwa mshindi? 2 Timotheo 4:7.

**MAONI**: Kila mtoto wa Elohim anapaswa kuwa ameridhika na maisha yake. Anapaswa kujua kila siku kwamba yeye hupigana vita vile vizuri vya imani.

8. Nini sasa ilikuwa ni faraja kubwa na tumaini kwa Paulo, na ni kwa wakati gani yeye aliangalia, akitarajia kupokea malipo yake? 2 Timotheo 4:8 [sehemu ya mwisho].

9. Nani alisimama na Paulo, na kumpatia nguvu za kupigana vita vya maisha? 2 Timotheo 4:17.

10. Paulo alikuwa na wasiwasi zaidi kuhusu ukombozi kutoka taabu au kutokana na kazi mbaya? 2 Timotheo 4:18.

11. Katika ushauri wa Paulo wa mwisho kwa Tito, nini yeye alisema kuhusu kukataa ubaya na tamaa? Tito 2:12.

12. Ni nini tunapaswa daima kuangalia kwa furaha na kutarajia? Tito 2:13: 2 Timotheo 4:8, [sehemu ya mwisho].

******************************